East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo

*Paul I. Mwiti Bundi[1*], Dkt. Onesmus Ntiba, PhD[1] & Dkt. Allan Mugambi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109 - 60400, Chuka, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: bundimwiti@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Octoba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Hadithi, Usasaleo, Teule.*

**IKISIRI**

Makala hii inachunguza mabadiliko katika hadithi fupi kwa mkabala wa usasaleo. Inaangazia athari za usasaleo katika hadithi fupi za kimapokeo. Kwa kuwa athari ya kiusasaleo inaendelea kujitokeza katika hadithi fupi za kisasa kila kukicha, kulikuwepo na haja ya kutafiti juu ya mabadiliko haya. Katika makala hii mtafiti alichunguza vile baadhi ya hadithi zilivyoegemea uhalisia na umapokeo na jinsi waandishi wengine walivyotumia majaribio ya kimuundo, kimtindo na kimaudhui kuandika hadithi fupi za kisasa. Mtafiti alikusanya data katika diwani tatu za hadithi fupi za: Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine na Homa ya Nyumbani na Hadithi Nyingine. Data iliteuliwa, kupangwa na kujadiliwa kulingana na maswali na madhumuni ya utafiti. Makala hii iliongozwa na nadharia ya umuundoleo iliyoasisiwa na Jacques Derrida na Michel Foucalt mwaka wa 1960. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa: Kubainisha mabadiliko ya kimuundo ya kiusasaleo katika hadithi fupi teule za Kiswahili, kudhihirisha mabadiliko ya kimtindo yaliyosababishwa na usasaleo katika hadithi fupi teule za Kiswahili na kufafanua mabadiliko ya kimaudhui yaliyotokana na usasaleo katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Katika hadithi sita teule zenye mbinu za kiusasaleo waandishi walitumia mabadiliko majaribio na upya katika muundo mtindo na maudhui. Sampuli maksudi ilitumika kuteua hadithi zilizofaa utafiti huu. Madhumuni na maswali ya utafiti yalitumika kuteua kupanga na kueleza data. Matokeo ya utafiti yalitolewa kimaelezo katika sura ya nne, tano na sita na hitimisha kutolewa katika sura ya saba. Matokeo ya utafiti yanatarajiwa kufaa wanafunzi wa fasihi wa shule za upili,watafiti wa baadaye, wahakiki na wasomi wa fasihi kwa kuwapa uelewa mpana wa mabadiliko yanayotokea katika uandikaji wa hadithi fupi za Kisasa. Zaidi ya haya, utafiti huu ulichangia kuziba pengo lililopo katika utafiti juu ya mabadiliko katika hadithi fupi mkabala wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

usasaleo. Maarifa yanayotokana na utafiti huu ni mchango muhimu katika fasihi andishi hasa hadithi fupi za Kiswahili.

**APA CITATION**

Bundi, P. I. M., Ntiba, O. & Mugambi A. (2022). Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 1-14. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882.

**CHICAGO CITATION**

Bundi, Paul I. Mwiti, Onesmus Ntiba and Allan Mugambi. 2022. "Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 1-14. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882.

**HARVARD CITATION**

Bundi, P. I. M., Ntiba, O. & Mugambi A. (2022) "Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 1-14. doi: 10.37284/jammk.5.2.882.

**IEEE CITATION**

P. I. M. Bundi, O. Ntiba, & A. Mugambi, "Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 1-14, Oct. 2022.

**MLA CITATION**

Bundi, Paul I. Mwiti, Onesmus Ntiba & Allan Mugambi. "Mabadiliko Ya Hadithi Fupi Teule Za Kiswahili : Mkabala Wa Usasaleo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Oct. 2022, pp. 1-14, doi:10.37284/jammk.5.2.882.

## UTANGULIZI

### Usuli wa Mada

Walibora na Mohamed (2015) wanasema kuwa mabadiliko na upya wa fani na maudhui huzuka mara kwa mara katika utanzu wa hadithi fupi za Kiswahili. Waandishi hawa wanaeleza kuwa kuna haja ya kuitazama upya dhana ya hadithi fupi hasa kwa kuzingatia njia ya mabadiliko ya fani na maudhui yanayoonekana katika matini za utanzu huu. Wanaendelea kufasiri kwamba baadhi ya waandishi na wasomi hupenda kusisitiza uhafidhina wa fani na maudhui ndani ya utanzu wa hadithi fupi. Wakifafanua zaidi wanasema kwamba tabia hii huonekana hasa katika fasihi changa au zinazoendelea pale wataalamu wanapojenga fikra ya kwamba hawahitaji kuzipa nafasi kazi zenye majaribio, mabadiliko na upya.

Kulingana na Ariel (1997) waandishi wa hadithi fupi za usasaleo wameamua ni vizuri hadithi fupi za kisasa kuzingatia mabadiliko ili kuleta upya. Mtaalamu huyu anasema uamuzi huu ulitokana na maoni kuwa wandishi wasipobadilisha mbinu za kimapokeo mitindo iliyopo itaanza kuchoshana na hatimaye itapuuzwa au kufa. Anazidi kusema kuwa hali hii inaonyesha waziwazi kwamba mabadiliko lazima yawepo ili yalete upya ndani ya matini ya hadithi fupi.

Minoo(1980) anaeleza kuwa umuhimu wa mabadiliko ni chachu ya kuisogeza mbele fasihi yoyote ile. Mtaalam huyu anazidi kufafanua kuwa pamoja na mfumko wa hadithi fupi kwa mtindo wa kimapokeo tayari kuna mikusanyiko ambayo imeandikwa kwa njia ya majaribio hasa katika misingi ya usasaleo. Anasema kuwa mabadiliko haya ya usasaleo ni njia ya utanuzi wa fikra ya dhana ya hadithi fupi za Kiswahili.

### Tapo la Usasaleo

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) tapo katika fasihi ni dhana inayotumika katika mazungumzo ya kifasihi kueleza kundi la wananadharia ambao wana mtazamo sawa kuyahusu masuala mbalimbali yanayohusiana na fasihi. Njogu na Wafula (2007) wanasema istilahi ya usasaleo ilitumika mara ya kwanza mwaka wa 1926 na B.I. Bell katika maandishi yake. Wanazidi kueleza wengine wanaosemekana kukuza tapo hili kama David Antin, Charles Oslon, John Cage na shule ya Ushairi na Sanaa ya Black Mountain College. Wanaeleza kuwa baadhi ya wanafasihi hulinganisha tapo hili na umuundoleo katika nadharia za kifasihi na kiisimu.

### Mitazamo ya Wanausasaleo

Njogu na Wafula 2007 wanaeleza mitazamo ya tapo hili kama ifuatayo; Wao hutazama ukweli kama kitu kisichoweza kuafikiwa na binadamu ingawa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

binadamu hujitahidi kuufikia. Aidha wanatapo hili hushughulikia masuala ya kifalsafa na kimetafizikia kama vile 'mimi' ni nani? Je Mungu yupo? Usasaleo huangazia baadhi ya vipengele vya kisimulizi vilivyokuwepo kwa muda mrefu. Waandishi katika kazi za kiusasaleo husawiri wahusika ambao kwa matendo na uhusiano wao; si wa kawaida Leger1990. Wao huwa na uwezo wa kutenda mazingaombwe kwa kuishi ulimwengu tofauti na wasomaji. Mitazamo hii ya usasaleo inahusiana na mihimili ya nadharia ya umuundoleo ambayo ni kati ya nadharia zinazotumika katika fasihi.

## MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umuundoleo. Wamitila (2003) anasema umuundoleo ni aina ya uhakiki inayohusishwa na wahakiki kama Jacques Derrida na Michel Foucalt. Anaendelea kuaeleza kuwa umuundoleo hutumiwa kama neno la kijumla la kuelezea aina mbalimbali za mikabala ya kifasihi na kifalsafa ya miaka ya Sitini (1960). Wao wanaeleza mihimili nadharia hii kama ifuatayo;

### Mihimili ya Umuundoleo

- Kushughulikia masuala ya kifalsafa na kimetafizikia.
- Kupinga kuwa kuna ukweli fulani katika matini za fasihi kwa vile nyumbufu isiyoweza kuafikiwa na binadamu.
- Kumpa msomaji uhuru wa kuchezea mawezekano ya kimaana katika matini za kifasihi. Hupinga kukamilika kwa jambo.
- Kuamini kwamba lugha ina uwezo wa kuzua maana nyingi.

## MUUNDO

Katika muundo hadithi za aina zote mbili zimezingatiwa katika makala hii ili kulinganisha muundo wa hadithi za kimapokeo na ule wa kiusasaleo.

### "Siku ya Mganga".

Hadithi hii ipo katika diwani ya "*Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine"* iliyohaririwa na K.W. Wamitila. Imeandikwa na Chesi Mpilipili. Hii ni hadithi yenye muundo wa kimapokeo. Mwanzo hadithi inaaza siku ya Jumamosi Mwaibale akijitayarisha kuanza kazi ya uganga. Kati anawashughulikia wateja wake wakiwepo wasomi waliotaka vyeo. Mwisho wembe ulioshughulikia wateja wake waathiriwa wa Ukimwi unamkata vibaya Mwaibale alipokuwa akikata makucha ya vidole vya mikono. Tunaachwa na taharuki ya kama atakufa au atapona. Huu ni muundo wa kawaida na wa kimapokeo usiozingatia vipandevipande vya matini kama mbinu ya usasaleo (Williams, 1995).

### "Jua Litawaka"

'Jua Litawaka' ni hadithi fupi iliyo katika mkusanyiko wa hadithi fupi unaoitwa "*Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine"*. Imeandikwa na Rebbecca Nandwa. Lengo lake ni kuonyesha matatizo yanayowakumba akina mama hasa katika ndoa. Mwanzoni msimulizi anaeleza shida zinazomkumba mwenzao Lina, kati Mama Ken, Beatrice au Betty, mellisa na Nana wote kwa hatamu wanapewa fursa ya kumshauri Lina; baadhi yao wakitumia maisha yao ya ndoa. Hadithi hii haifikii mwisho wa kawaida kwani hatujaelezwa kama Lina na mumewe wanarudiana au vile maisha ya Lina yanaendelea baada ya hapo. Muundo huu ni ule wa usasaleo wa vipandevipande vya matini. Katika muundo huu kuna wazo kuu linalounganisha vitushi. ( May, 1994). Hili ni shida katika maisha ya ndoa. Katika muundo wa vipandevipande vya matini hadithi huwa haina mtiririko wa moja kwa moja kiwakati au kinafasi( Minoo, 1980).

### "Njaa"

Hadithi ya "Njaa" iko katika mkusanyiko wa hadithi wa *"Homa ya Nyumbani na Hadithi Nyingine"* (2004, uk.140). Imeandikwa na Baingana. Muundo wa hadithi hii ni wa kiusasaleo wa vipandevipande vya matini. Haina mfululizo au mtiririko wa moja kwa moja. Hadithi za aina hii huwa na uhusika wa wahusika mbalimbali au mshikamano wa vipengele fulani vya njia za hadithi fupi husika (Walibora na Mohamed, 2015).

Hadithi hii imekunjuka kwa mfuatano wa wakati ikisimulia matukio katika nyakati tofauti. Hadithi za vipandevipande huwa na useja unaounganisha matukio Sullivan na Nancy (1981). Useja wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

matukio katika hadithi ya "Njaa" ni hali ya Patti Mugisha shuleni Gayaza siku ya Jumapili tarehe kumi kutoka saa nane hadi saa nne na nusu usiku.

Mbinu hii ya vipandevipande vya matini imewezesha Patti kusimulia hadithi kadhaa. Hadithi hizi ni: Wazazi wa Patti kukosa kumtembelea shuleni, hali ya vyakula shuleni na uhusiano wa Patti na wanafunzi wenzake Linette na Maria pale shuleni. Msuko hauna mtiririko wa moja kwa moja. Mbinu inayotumika ni ya Shajara ya Jumapili hii. Huu ni muundo wa usasaleo.

## MTINDO

### "Kachukua Hatua Nyingine"

Hadithi hii ipo katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyinginie*. Ina mtindo wa kimapokeo.

#### *Usimulizi*

Katika 'Kachukua Hatua nyingine' Wamitila anatumia msimulizi wa nafsi ya tatu. Usimulizi huu wa nafsi ya tatu unaifanya hadithi kuwa na masafa ya ujumi marefu Arega na Wenzake (2012). Msimulizi anajua kila kitu. Ana uwezo wa kuwa kila mahali. Anatujulisha yaliyo katika nafsi ya Shemeji Sakina. Aghalabu hadithi nyingi za usasalaeo husimuliwa kwa nafsi ya tatu. Hii ni hadithi ya mtindo wa kimapokeo.

#### *Istiara*

Maandishi ya kiusasaleo huhusisha Istiara iliyotiwa chumvi mno (Traore, 2015). Lakini katika hadithi hii istiara ya kawaida inatumika kutoa ulinganisho wa moja kwa moja. Wakati shida ilipokumba jamii ya Mavitu Serikali ilikuwa na chakula cha kuwasaidia watu kupambana na njaa "*iliyokuwa ikiwatanulia mabawa na kuwakondolea macho"* (2004,uk.40). Hapa njaa inalinganishwa na bundi. Katika jamii ya Waswahili bundi huashiria mambo hatari kwa binadamu.

#### *Takriri*

Huku ni kurudiarudia kunakotumika katika maandishi ya kifasihi kwa nia ya kukaza, March (2009). Ubishi baina ya mke wa Mwajiri na Sakina umetiliwa mkazo kwa takriri ya maneno "Walipinga", "alibisha" na "vuta ni kuvute" (2004, uk.46).Hadithi yenyewe imerudiarudia maneno "alichukua hatua nyingine" au "kuichukua hatua nyingine" Amata (2005). Marudio haya ni tofauti na yale ya usasaleo ambayo hurudiarudia neno, kiambishi au sentensi mara kadhaa kwa lengo la kusisistiza, King'ei (2005). Marudio haya yanazingatia mhimili wa umuundoleo kwamba lugha huweza kuzua maana nyingi.

#### *Wahusika*

Wahusika ni watendaji katika kazi za kifasihi. Wao hutenda na kuhusiana na wengine ili kuwasilisha maudhui na dhamira ya mwandishi; Iribemwangi (2011). Katika hadithi hii, wahusika ni wa kawaida: Ni wale wanaoishi katika ulimwengu mmoja na msomaji. Hawatendi maajabu au Mazingaombwe kama baadhi ya wahusika wa usasaleo.

### "Mayai Waziri wa Maradhi"

#### *Wahusika*

Wahusika ni watendaji katika kazi za kifasihi (March, 2009). March anaeleza kuwa mwandishi huwatumia kutenda na kuhusiana na wengine ili kuafiki dhamira na maudhui yake. Baadhi ya wahusika wanaozingatia mbinu za usasaleo hutenda mambo ya ajabu (Giddens, 1990).

Mwandishi ametumia wahusika ambao hawaishi katika dunia ya kawaida. Ukombozi aliyeaga dunia miaka minne iliyopita anaingia jumbani. Anakuja na watoto wengine tisa. Mizuka hii inafanya maajabu. Inajifungulia mlango na dirisha, inakula na kuosha vyombo. Inakuja na vitabu vya 'Azimio la Arusha' na sera nyingine. Mizuka hii inapuuzilia mbali mawaziri wote, ila mmoja kisha wabunge wote bila kumbakisha hata mmoja. Inaamsha fikra za mazingaombwe na ushirikina.

Mayai ni Waziri wa Maradhi anazionea fahari picha zinazomwonyesha akizindua majengo ya kuendeleza maradhi mbalimbali. Ni waziri yupi wa kawaida atasifu kipindupindu na kifua kikuu kuwa ni maradhi yanayosaidia kupunguza idadi ya watu? Wahusika ambao hawaishi katika dunia ya msomaji ni msingi wa usasaleo. Mambo ya kimetafizikia na kifalsafa pia ni mhimili wa umuundoleo. Mfano wa dhana hii ni mizuka iliyomkabili Mayai. Hii ni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

mizuka ya watoto kumi akiwepo mtoto wake Mayai; Ukombozi.

***Maono na Ndoto***

Maono ni picha ya mambo au vitu inayomjia mtu bongoni mwake ( Mohamed, 2001). Okombo (1992) anaeleza ndoto kuwa maono yanayotokea usingizini. Mwandishi anatumia maono kutukuzia maudhui ya mizimu. Mayai anaona mlango ukifunguka ilhali aliufunga kwa ufunguo kisha anaona dirisha likifunguka. Anamwona mwanawe marehemu Ukombozi. Halafu anaona dirisha likifungika. Mayai anaona mizimu ( mizuka) ikitembea na kula.

Ndoto zimetumiwa kukuza maudhui ya mizuka. Inaenda pamoja na maono. Mayai anapoenda kulala mchana anaota yeye na mawaziri wenzake wakila na kulewa . Ndoto na maono ni njia ya usasaleo ya kusimulia hadithi (March, 2009). Aghalabu huambatana na mazingaombwe na wahusika wasioishi katika ulimwengu wa wasomaji.

***Mtiririko wa Fikra Tambuzi***

Hii ni mbinu ya kimtindo ya kiusasaleo ambapo mawazo hutirirka kutoka kwa msemaji , msimulizi au mwandishi. Si lazima msemaji azingatie alama na kaida nyingine za lugha (Stuart, 1998).

> *Mambo yalianza. Kina Mwinamila na Makongoro walionyesha ufundi wao. Ngonjera zilicheshwa, mashairi yaliimbwa . Mzee Moris alipiga ngoma zake kumi na baadaye watoto kumi waliozaliwa siku ya uhuru walionyeshwa. Watu wakashangilia.*

***Mzaha wa Maneno***

Hii ni mbinu ya kimtindo ya usasaleo ambapo maneno huweza kuchochea maana isiyoweza kufikirika na isiyo ya kawaida; aghalabu hustajabisha na kuchekesha . ( Sandra, 1985).

> *Mwishowe aliufikia ule ukurasa alioupenda kuliko zote. Picha nyingi kati ya hizi alikuwa akizindua majengo ya kuendeleza maradhi mbalimbali kama kipindupindu na kifua kikuu kwa kuwa yanasaidia kupunguza idadi ya watu duniani. Katika baadhi ya picha alijiona amekaa ndani ya gari akiendesha. Kama Waziri alikuwa amepitia Wizara nyingi. Alianza wizara ya elimu na mchakamchaka, akahamishwa Wizara ya biashara na milungula na sasa alikuwa waziri wa maradhi***.*** *Picha hizi alizitazama kwa muda mrefu halafu akafunua ukurasa uliofuata(*2004, uk.65).

Maneno ya kimzaha yanatumika na Kezilahabi hapa ili kudhihaki siasa za nchi za Afrika ya Mashariki ambako mawaziri na viongozi hawahudumii wananchi ipasavyo. Huu ni mzaha wa maneno uliokithiri. Umuundoleo huamini kuwa lugha ina uwezo wa kuzua maana nyingi. Mzaha wa maneno hapa umetumika kudhihaki sera za uongozi katika nchi za kiafrika.

***Mseto wa Ndoto, Uhalisia na Mazingaombwe***

Waandishi wa kiusasaleo huchanganya ndoto na uhalisia katika hadithi yenye mazingaombwe ili kuzuia kukera wasomaji au viongozi. Maelezo huwa na ibura na mambo yenye utata ambayo hayawezi kufasiriwa moja kwa moja. Hujishughulisha na masuala ya kimetafizikia na kifalsafa ambao ni mhimili wa umuundoleo.

Mayai anaota wakikojoa mtoni sehemu ya juu, chini bondeni wakulima walikuwa wameweka majembe yao pembeni mtoni, wakioga na kusugua miili yao kwa mawe. Wanawacheka wale wakulima; hawa ni viongozi wasiojali walio chini yao.

> *Akiwa kitandani ndoto za mchana zilianza kumsumbua. Ndoto ya kwanza aliota yeye na mawaziri wengine pamoja na wabunge kadhaa wakiwa ndani ya baa wakinywa pombe. Chupa zilikuwa zimejaa mezani na kezi nyingi zilikuwa zimepangwa pembeni zikiwasuburi* ( 2004, uk.73).

Wakulima katika nchi za kiafrika huchangia nchi zao kiuchumi. Hawafai kudharauliwa na viongozi wa nchi na kuchekwa kwa sababu ya hali yao duni. Wanafaa kushughulikiwa kiuchumi. Mwandishi akifafanua hili anasema: Mayai alisoma gazeti la uhuru ambapo barua ya kwanza ilisema hivi:

> *Tanzania ilikuwa katika majira magumu zaidi ya kujenga ujamaa: Unafiki umezidi na hali ya kutojali ilikuwa imeenea mioyoni mwa watu. Barua hii aliruka akasoma nyingine . Nayo ilikuwa ikiwatetea wakulima. Ni wazi kuwa mji wa Dar es Salaam umebadilika, mji wa Mwanza*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

> *umebadilika. Lakini hali ya mkulima haijabadilika…* (2004,Uk. 66)

Hapa kwa njia ya ndoto mwandishi ameweza kueleza ukweli wa hali ya wakulima katika nchi ya Tanzania. Mazingaombwe yametumiwa na mwandishi ili kuonyesha hali ya wananchi katika nchi ya Mayai Waziri wa Maradhi. Saa sita ya usiku Mayai anatembelewa na mizimu ya watoto kumi akiwemo marehemu Ukombozi. Mayai anawashuku wazee waliomzika mwanawe kuwa waliomfanyia mazingaombwe. Saa kumi Usiku mzuka wa Ukombozi unarudi ukiwa na mizuka mingine ya watoto tisa wakondefu waliovaa matambara. Ukombozi anavaa vizuri lakini afya yake si nzuri. Ukombozi anawahudumia wale watoto kwa chai, mikate na vyakula vingine.

***Mchango wa Vyombo vya Habari***

Vyombo vya habari, magazeti na simu vimechangia sana katika kuleta mwamko mpya wa usasaleo( Myszor, 2001). Mayai Waziri anaposoma gazeti la "*uhuru"* anasoma barua kuona vile wananchi wanasema juu ya Wizara yake. Inaonekana anachelea yoyote mabaya ambayo yangekuwa yameandikwa.

> *"Baada ya chai mfanyakazi wake amekwishamletea gazeti la "Uhuru". Waziri alilipitia haraka haraka. Mara nyingi alipendelea kutazama kwanza barua za wasomaji ili kuona kama kuna manung'uniko yoyote kuhusu wizara yake" ( 2004, uk. 70 - 71).*

Magazeti ni chombo cha mawasiliano kinachotumika katika enzi ya usasaleo kuwazindua watu, ili watetee haki zao. Hapa wakulima na viongozi ndio walengwa. Simu kadhalika ni chombo kingine kinachoweza kutumiwa kuwatetea wanaokandamizwa ili wasaidiwe. Mayai anawaita polisi anaposumbuliwa na mizimu (2004, uk. 65).

**'Mizungu ya Manabii'**

Hadithi hii ni mojawapo kati ya hadithi zilizoteuliwa ili kuonyesha mabadiliko majaribio na upya unaoshuhudiwa katika hadithi za usasaleo. Ina vipengele kadhaa vya kimtindo.

***Usimulizi***

Mwanzoni mwa hadithi msimulizi anatumia nafsi ya tatu kutanguliza. Nafsi ya kwanza imetumika kwa kiasi kikubwa kusimulia hadithi hii. Hata hivyo mbinu ya kutumia alama za usemi halisi ndiyo inatawala. Usimulizi wa nafsi ya kwanza aghalabu hushuhudiwa katika maandishi ya usasaleo.

***Mdondosho***

Bates (1941)anasema hadithi fupi ya kisasa inatumia mbinu hii ya usasaleo ambayo husimamia usemi ambao humtoka, msemaji mfululizo Aghalabu mbinu hii haizingatii kanuni za matini - kwa mfano muundo kamili wa sentensi.

> *Anakumbuka miaka mitatu iliyopita. Alipojiunga na dini hii ya siri. Aliyaona matendo ya kutisha yaliyoambatana na matambiko ya sadaka za damu ya binadamu na hasa wasichana bikira, yalimtia hofu na kumpaza usingizi*. (2010, uk. 36)

Mdondosho huu ni maelezo ya msimulizi yanayoonyesha hali ya wanachama wa Global Youth Cultural Centre pale wanaposhuku kwamba lengo lao la kukubaliwa kwa mtandao huu wa siri wa kueneza ukoloni mambo leo halitafaulu.

***Utata***

Utata unatokea hadithini pale yanayoelezwa si wazi kimaana ( Mvati, 2010). Hii ni mbinu nyingine ya kimtindo katika usasaleo iliyotumika. Mbinu hii inatoa mwanya zaidi kwa wasomaji kutofautiana katika kujenga maana ya kazi husika (Ariel, 1997).

Utata unatokea pale Maimuna alipoonja damu ya Rais na kusogelea Kibwengo na kupiga magoti. Aliupaka mwili wote wa kibwengo damu hiyo. Ghafla jengo lote lilitetemeka. Kibwengo polepole aligeuka roho na kupaa, akatoweka machoni pao. Alienda hospitali ya Tower of Babel akatoa roho ya Rais Mutinda. Mambo haya hayaelezeki kwa njia moja kwa kutumia akili za binadamu. Utata hutumika katika maandishi ya usasaleo pale inapokuwa mambo yanayotendwa na mhusika hayawezi kueleweka; Si ya kawaida kutendeka. Huhusisha falsafa au metafizikia. Mhimili wa umuundoleo husema kuwa utata humpa msomaji uwezo wa kuzua maana nyingi kutoka maelezo.

***Uvijembe***

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

Maelezo yenye mafumbo na ambayo hayasemi kitu moja kwa moja katika hadithi ndiyo hali ya uvijembe; Ballard (1991). Kulingana na Sacido (2012) uvijembe ni njia ya Waandishi katika enzi ya usasaleo kukejeli tukio tabia au kitu kwa njia isiyoudhi. Katika Mizungu ya manabii, Kezilahabi anatumia Komosa, Wabunge na Rais Mutinda kusimamia viongozi wa nchi za kiafrika ambao hushawishiwa na kukubali nchi zao kunaswa katika mfumo wa unyonyaji wa ukoloni mamboleo. Rais Mutinda anashawishika baada ya kudinda kwa muda mrefu. Waziri wake wa utamaduni, Komosa anakubali haraka baada ya Kuhongwa na kuahidiwa kuvundikiwa madola zaidi katika mabenki ya Uswizi.

***Wahusika***

Baadhi ya wahusika hawezi kuishi katika ulimwengu tunaoishi. Si wa kawaida kwa vitendo na mienendo yao. Yola alikuwa kuhani na nabii mkuu wa hekalu la dini ya Siri huko Madrid. Ndiye aliyetia damu ya Rais Mutinda ndani ya bakuli kisha akaichanganya na aina aina ya mavumba akaanza kutabana ndipo wengine wakajiunga naye katika hayo manuizo. Alichukua chupa ya mafuta ya mzeituni akayamimina ndani ya bakuli; aliichanganya mara kadhaa akaichovya kidole cha Shahada na kuramba. Damu hii ni ya mtu aliye hai na ni ajabu kwani inarudishwa kwake huku akikubali kadhia ya kuanzishwa Global Youth Cultural Centre iliyofikiriwa angekataa. Kibwengo na Maimuna ni majini waliokuwa na uwezo wa kujibadilisha wakawa binadmau wakati wowote walipotaka.

Mojawapo kati ya mitazamo ya usasaleo uhusuo mabadiliko katika fasihi ni kuwa waandishi hutumia wahusika wasio wa kawaida. Hawa hutenda mambo ambayo hatuwezi kuyatenda tukiwa binadamu. Wahusika hawa wawili ni wa aina hii.

***Mazingaombwe***

Mazingaombwe hadithini ni tukio ambalo humfanya mtu aone mambo yasiyo ya kawaida kutendeka ( Stuart, 1988).

Mbinu ya kusimulia hadithi mwandishi akihusisha mbinu ya mazingaombwe ni ya Usasaleo(Sacido , 2012) Mbogo ametumia mbinu hii kuashiria ujanja wa wazungu wanapotaka kutawala nchi kiuchumi katika ukoloni mamboleo. Mbali na kuhonga viongozi kama mawaziri, wao hulazimika kutumia mbinu nyingine kwa wale wasioshawishika kwa urahisi.

Kibwengo na maimuna ni majini wawili kutoka nchi za kiarabu wao wana uwezo wa kujibadili na kuonekana kama binandamu. Walitumia mbinu za kiajabu kumshawishi Rais Mutinda kutia sahihi mkataba wa kujenga GYCC katika mwa mji. Wanatenda maajabu yasiyoaminika.

> *Kibwengo alivua nguo akabaki uchi wa mnyama. Alikwenda akalala chali mbele ya kuhani Yola. Yola aliitia damu ya Rais Mutinda ndani ya bakuli kisha akaichanganya na aina kwa aina ya mavumba. Alipoanza kutabana wengine wote walijiunga naye katika manuizo* (2010, uk. 48).

Yanayotokea hapa si kawaida. Majini wanajibadili na kuwa binadamu. Wanachezea damu ya mtu badala ya kuipima kujua ugonjwa. Wanaichanganya na mafuta ya mzeituni na kuionja. Jengo lote linatetemeka Kibwengo anageuka roho na kuonekana katika runinga akienda hadi hositali alipokuwa Rais Mutinda. Haya yote ni mazingaombwe na ambayo binadamu hawezi kuyaamini.

***Magazeti na Utandawizi Kutumika Kutoa Taarifa***

Matumizi ya vyombo vya habari kuwaarifu watu mambo yanayotokea katika nchi yao na kuwazindua ni dhamira ya usasaleo.

> *Gazeti la jioni "The speaking drums of Afrika", siku ile ile lilitoka na kichwa cha habari: PRESIDENT SIGNS GYCC CONTRACT* (2010, uk. 55).

Vyombo hivi hutumika kuwazindua watu ili wajue yanayotokea na ikiwezekana waweze kutetea haki zao. Kutetea haki za wanyonge ni dhamira ya usasaleo (Stuart, 1998).

***Mseto wa Uhalisia, Bunilizi na Mazingaombwe.***

Hadithi hii inahusu ukoloni mamboleo na kuingizwa kwake katika nchi za Kiafrika. Katika nchi ya Komosa, waziri wa utamaduni, mjadala kuhusu kuanzishwa kwa GYCC ulizua zogo miongoni mwa wasomi na vyombo vyote vya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

habari. Mbunge mmoja alilalamika kuwa ilikuwa njia ya kuleta ukoloni mamboleo. Mwingine alimwonya dhidi ya kuharibu vijana. Baada ya kuvundikiwa madola katika mabenki kule Uswizi Komosa anajaribu kila njia kushawishi wabunge na wananchi kukubali kuanzishwa mradi wa GYCC katika nchi.

> *" Lufasi keshatoa amri ifikapo 2020", alisema Nixon. " Kila mji mkubwa kusini mwa jangwa la sahara sharti uwe na GYCC . Mtandao huu hatimaye utaunganishwa na ule wa Asia , Ulaya na Marekani ya Kusini. Na hapo ndipo tutakuwa tumeikamata dunia na kuudhibiti uchumi wa ulimwengu wote na kuwatia kitanzi watu wa dunia ya tatu*"( 2010, uk. 37).

Nukuu hili linadhihirisha kuwa lengo la GYCC lilikuwa kueneza unyonyaji wa ukoloni mamboleo katika nchi za ulimwengu wa tatu zilizoko Afrika, Asia, Ulaya na Marekani ya Kusini.Hii ni hadithi ya kubuni inayogusia ukweli wa nchi za dunia ya tatu kunaswa katika mtego huu. Mgogoro wa hadithi ni kukataa kwa viongozi mwanzoni kukubali kuanzishwa kwa mfumo wa GYCC. Kati hadithi ina maelezo ya vile Rais Mutinda anashawishiwa kimazingaombwe kukubali na kutia sahihi mkataba wa kuanzishwa GYCC katika nchi yake.

Mwishowe Rais anatia sahihi kuanzishwa kwa GYCC. Hii ni hadithi ya kubuni yenye muundo wa kawaida wa hadithi fupi ulio na mwanzo kati na mwisho. Kuna mazingaombwe yanayotendwa na Maimuna, Kibwengo na Yola. Haya ni matendo yasiyoweza kutendwa na mhusika wa kawaida. Kibwengo anajipenyeza ndani ya gofu la mwili lisilokuwa na roho, na kuendelea kulala usingizi. Haya ni mazingaombwe yasiyowezekana na binadamu wa kawaida. Kuchanganya ukweli na mazingaombwe ni mbinu ya usasaleo.

### Mtindo katika "Jua Litawaka"

Hadithi hii iko katika mkusanyiko wa hadithi Ulio katika kitabu cha "*Mizungu ya Manabii na hadithi Nyingine".*

#### *Usimulizi*

Msimulizi anafanya hivi kwa nafsi ya kwanza. Ni hadithi ya mtindo wa vipandevipande vya matini. Anasema kuwa anawaalika wanawake wengine wamshauri na kumfariji. Hadithi nyingi zenye mabadiliko na usasaleo husimuliwa katika nafsi ya kwanza.

#### *Mdondosho*

Mabadiliko ya usasaleo ndani ya hadithi fupi za kisasa yana mtindo wa lugha ambao ni mdondosho na mkato ( Sandra, 1985). Mwandishi huyu anaeleza kuwa mdondosho ni usemi unaoandikwa mfululizo na wakati mwingine haujali kaida za lugha kama vile alama za usemi halisi au kaida za kuunda sentensi.

Msimulizi anaanzia kwa mbinu ya mdondosho.

> *Ulimwengu umempasukia biandamu. Nafasi yake yakereka. Tumbo limejaa joto. Hali halali kichwa Chamuuma akitia akitoa. Kufikia sasa hajapata suluhisho jahazi la Lina lisizame* (2010, uk.190).

Huu ni utangulizi unaolengwa kueleza hali mbaya ya Lina baada ya kuharibikiwa na ndoa yake. Mbinu hii imetumika ili kueleza mambo mengi kwa mkato kumfanya msomaji aendelee kusoma hadithi akijua asili yake.

#### *Kurudiarudia*

Mbinu hii hukariri viambishi maneno, vifungu vya maneno, vinyume vya maana au sentensi, Amata (2005). Maelezo ya Lina yana urudiaji. Marudio haya yanazingatia kiambishi cha nafsi ya kwanza "Ni"

Mbinu ya kiusasaleo ya kukariri kwa kurudiarudia maneno, vifungu vya maneno, kwa kutumia vinymue imetumika na Nana katika mazungumzo yake.

> *Vileo hivyo vilimduwaza na kumfufumaza akili tu kwa muda kila kulipokucha na kuchwa uraibu wake ulikita mizizi na kuwa Sugu. Ulifika kiwango ambacho*(2010, uk. 93).

Maelezo haya ya Nana yanatumia takriri ya maneno na vinyume ili kukaza juu ya umuhimu wa kuvumilia na kujipoza katika maisha ya ndoa yenye shida. Anasema kukata tamaa na kuendea ulevi ni kujiangamiza mwenyewe. Lengo la urudiaji huu ni kusisitiza au kukaza ili kuonyesha ni yeye binafsi aliyekumbwa na kadhia hizo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

**"Zawadi ya Mume Wangu"**

***Takriri***

Takriri huhusu kurudiarudia. Hii ni mbinu ya usasaleo. Maandishi mengi ya usasaleo huwa na urudiaji (Sacido, 2012).

> *Hebu fikiria uzito wa kazi ya mwanamke kama mimi ninayeamka alfajiri kuosha vyombo vilivyolala. Ninayefagia ndani na nje ya kibanda changu cha uchwara. Ninayetayarisha kifungua kinywa cha mihogo na chai ya mkandaa* (2015, uk. 10).

Kidawa anazungumza kusisitiza vile analazimika kufanya kazi nyingi za sulubu. Anasisitiza kuwa yeye ndiye anatekeleza majukumu haya yote bila kusaidiwa na yeyote. Hadithi hii imeshughulikia utetezi wa haki za wanawake ambayo ni dhamira moja ya usasaleo. Kidawa ametuchorea hali yake ya kuachiwa majukumu yote ya nyumbani na mumewe Bakari Kadaku. Hata anapokuwa nyumbani

***Sitiara Iliyotiwa Chumvi***

Sitiara ni ulinganisho wa kitu au mtu moja kwa moja bila ya kutaja sifa ya ulinganisho (Amata, 2005). Akieleza, Sitiara iliyotiwa chumvi Traore(2015) anasema kuwa Sitiara hii hupigwa chuku na kufanya jambo au kitu kupewa uwezo usio wake mara nyingi. Mbinu ya ishara na sitiara iliyotiwa chumvi mno ni mbinu mojawapo ya usasaleo katika hadithi fupi za Kiswahili.

> *Wakati wote huo ndege hunizunguka na kunishangilia. Nimewakaribisha ndege wanizoee kwa nini wasinishangilie? Wao pia wamenizoea. Mazoea zaidi ya yale ya mume wangu aliyeyoyoma na kunikimbia. Ijapokuwa yalikuwa mazoea ya sehemu ndogo tu. Sehemu ndogo tu kama punje ya mchanga. Mazoea ya ndege na binadamu huweza kumjaza mtu furaha* (2015, uk. 14).

***Kurudiarudia***

Kurudia kunakojenga muziki au mchezo wa maneno na sauti ni mbinu ya usasaleo. Kinachorudiwarudiwa huwa viambishi,vifungu au sentensi.Mbinu hii inadhamiriwa kusisitiza dhana, fikra au ujumbe unaotolewa katika matini (Wamitila, 2008). Mfano mwingine unapatikana katika hadithi ya Said.A.Mohammed 'Tazamana na Mauti' katika mkusanyiko wa *"Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine"*

> *Leo Lucy anapitapita jijini tu kama anavyopita siku zote. Macho yake yanatazama nyuso za wazungu,vijana na wazee. Si kuwatazama tu, bali kutabasamu nao. Si kutabasamu tu bali kutabasamu kwa namna ya kutabasamu huku akiwacha tabasamu yake imemganda mzungu moyoni mwake* (2007, uk. 92).

***Utata***

Walibora na Mohamed (2015) wanaeleza kuwa mbinu hii huwa inatumika pale waandishi hawatoi maelezo ya moja kwa moja au waziwazi. Huhitaji utapta kwa kuwa na mwanya zaidi kwa wasomaji kutofautiana katika kujenga maana. Umuundoleo humpa msomaji uhuru wa kuchezea mawezekano ya kimaana.

> *Hapo huyo mwanamke aligeuka kunipa mgongo. Akakupuka bila kutazama nyuma. Ilikuwa vigumu kwangu kutambua kama ile ilikuwa ndoto au ukweli?* (2015, uk. 15).

Maelezo haya ya kidawa yanaonyesha utata. Hajui kama mwanamke aliyemkabili alikuwa binadamu au shetani. Badala ya kukamilisha maelezo yake kwa kueleza yeye ni nani anamwacha kidawa akibahatisha. Alipouliziwa kujitambulisha alimwachia kutafuta majibu ya swali lake ambalo lilikuwa vigumu kutatua.

***Mazingaombwe***

Mazingaombwe ni mbinu ya usasaleo iliyotumika katika hadithi hii. Hapa mambo yanayotendeka huwa si ya kawaida na humwacha msomaji na maswali mengi yasiyojibika ( Sacido 2012). Kidawa anasema kwamba aliwatia ndege moyoni mwake ili wajaze lile pengo la mume wake aliyetorokea mjini. Anaeleza kuwa ndege nao walimtia nyoyoni mwao wakawa na uhusiano wa kirafiki. Hili si jambo la kawaida katika maisha ya kila siku.

> *Wakati wote ndege hunizunguka na kunishangilia. Nimewakaribisha ndege wanizoee kwa nini wasinishangilie?. Wao pia*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

> *wamenizoea mazoea zaidi ya yale ya mume wangu* (2015, uk. 14).

Kidawa anakabiliana na mwanamke ambaye alikuja kwake kumdodosa. Kulingana na maelezo yake mwanamke huyu alikuwa kiumbe cha ajabu. Anamweleza kama kiumbe ambaye alikuwa hajamwona katika maisha yake. Wororo wa ngozi yake, alivyojipodoa na kujirembesha kunamfanya Kidawa amwote katika ndoto au katika vitisho na vituko vya jinamizi ( 2015, uk.19).

***Mwigo wa Kuchekesha***

Hii ni dhamira mojawapo katika usasaleo. ( Ariel, 1997) mwigo wa kuchekesha, hutumiwa katika maelezo au mazungumzo kwa njia inayoweza kuzua ibura na ucheshi.

***Mtiririko wa Fikra Tambuzi***

Ni mbinu ya majaribio ambayo ilianzishwa na William James mwaka wa 1890 katika andishi lake la *Misingi ya Saikolojia* na baadaye kutumika katika uwanja wa fasihi hasa katika tanzu za riwaya na hadithi fupi miongo ya mwanzo ya karne ya ishirini Walibora na Mohamed (2015). Huibua na kushika fikra zinazopita bongoni na hisia za undani nafsini zinazojitokeza katika maisha ya kila siku.Aghalabu haijali kaida za kuweka vituo vya uandishi au alama za usemi halisi. Katika hadithi ya "Zawadi ya Mume Wangu" Kidawa anasema:

Mbinu hii imetumika katika hadithi ya "Mwanzo wa Mwisho" katika mkusanyiko wa *"Homa ya Nyumbani na Hadithi Nyingine".*

> *Sasa nisingeweza kujibereuza wala kujibabaisha tena. Tiba aliyekuwa kijiba, cha roho nilimtaka ukomo wa kumtaka! Nilikuwa hivyo.*

Haya ni maelezo ya mhusika mkuu Hamidu. Alikuwa amemtamani sana msichana aliyeitwa Tiba mfanyikazi *mwenzake* hotelini. Siku hii alijitia ujasiri hadi kumwambia. Alipokataliwa alianguka na kuzimia hadi asubuhi ya siku iliyofuata. Inavyoonekana katika dondoo hii hakuna umakini katika matumizi ya kaida za kuweka alama za tamko la moja kwa moja.

**"Njaa"**

Hadithi hii iko katika mkusanyiko wa hadithi fupi uitwao. "*Homa ya Nyumbani na hadithi Nyingine".*

***Usimulizi***

Patti anapozungumza katika sehemu nyingi anatumia nafsi ya kwanza. Hadithi fupi ambazo husimuliwa katika masafa.

***Mdondosho***

Mbinu hii imetumika na Doreen Baingana katika hadithi hii:

> *Chai yangu sasa ilikiwa ya uvunguvungu na yenye utamu wa kuchukiza ulioumiza koo yangu lakini niliilazimisha kupita kooni. Sikuwa nikisoma ila kuwaza . Ah Mungu! Vipi wewe una upendeleo! Unawezaji kumpa mwovu vyakula vyote na vitu alivyo navyo? Mbona nilijitesa kwa kurudi bwenini kunywa chai?* (2015,uk.146).

Haya ni maneno ya Patti akizungumzia hali yake ya kukata tamaa na aibu baada ya ushuhuda katika ukumbi wa Kanisa. Hii ni mbinu ya usasaleo ya mdondosho na mkato. Patti anaeleza uhusiano wake na Linette na Maria. Huu ni mfululizo ambao kupitia kwake tunaelewa vile alikuwa akitamani kuwa kama mtoto wa tajiri ambaye ni Linette.

***Kurudiarudia***

Patti anakaza hali yake ya kuchoka na kuamua kuelekea ukumbi wa kanisa kumcha Mungu tu. Anaona kuwa ahueni ingepatikana kutoka kwa Mungu tu. Mambo ya ulimwengu hujaa usumbufu usiokoma.

Takriri inapatikana katika nukuu hili:

> *Nilihisi kuemewa zaidi na maisha na njaa; njaa ya chakula, njaa ya roho mtakatifu njaa ya kutengwa na kundi hili la waumini, madada zangu katika Kristo, njaa ya kutengwa na wasichana wengine bwenini, njaa; njaa ya kutaka kuwa sehemu ya kitu fulani* (2015,uk. 149-150).

Takriri hii ya neno "njaa" nimsisitizo haja na mahitaji aliyokuwa nayo Patti ambayo aliomba

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

Mungu amsaidie kuyakidhi. Alikuwa na haja ya kiroho, kuondokewa na shida za umaskini, kutotengwa na wengine na hata aila yake kutomtembelea shuleni. Mhimili wa umuundoleo wa "Ukweli usioweza kuafikiwa" yanajitokeza katika usaili wa Patti kuhusu imani yake.

***Metafizikia***

Metafizikiwa huhusu haja ya uchunguzi wa kindani ili kujua asili ya mambo mengi yahusuyo ulimwengu na uwepo wa Mungu na binadamu (Farhat, 2003). Hushughulikiwa katika usasaleo na umuundoleo.

Patti anasaili uwepo wa Mungu na kumlaumu kwa mapendeleo na maonevu kwa kuonekana anayebagua watu wake.

> *Nyakati nyingine ni vigumu kumwamini Mungu, hasa nikifikiria mambo anayonipitishia. Na husema ananipenda. Nilirudi bwenini wakati wa chai, kwa vyovyote vile kwa sababu nilikuwa na njaa sana: Nilimwamini Mungu kwa miujiza (yake). Kwa nini nisimwamini? Mimi ni mtoto wake; mtoto mteule* (2015,uk.143).

Wanametafizikia husaili uwepo wa Mungu (March, 2009). Patti anaonekana ana imani ya Mungu lakini isiyo dhabiti. Ana dukuduku kuhusu tabia ya Mungu na kumwona kama anayebagua watu wake. Jambo hili linahusisha muundo wa umuundoleo wa falsafa na metafizikia.

**MAUDHUI**

Sehemu hii katika makala hii inatumika kulinganisha maudhui katika hadithi nne. Moja yenye maudhui ya kimapokeo na tatu zenye maudnhui za mabadiliko majaribio na upya wa kiusasaleo. Hadithi zilizo nyingi zimetumika upande wa usasaleo ili kutoa mifano maridhawa.

**"Kikojozi"**

Hii ni mojawapo kati ya hadithi kumi na mbili katika diwani ya Mizungu ya *Mababii na Hadithi Nyingine*. Maudhui zake zimeshughulikiwa kimapokeo.

Dhamira ya jinsia kwa kutetea haki za wanawake ni ya usasaleo. Katika hadithi hii mwanamke anadunishwa. Huu ni mtazamo wa umapokeo kwamba mwanamke anafaa kungozwa na mwanamume kwa kila jambo. Umuundoleo huhimiza kushughulikia masuala ya kifalsafa na undani wa mambo kama haki za wanawake katika jamii. Mwandishi anaonyesha kuwa mwanamke ana haki ya kujiamulia mazuri na mabaya. Kupigwa kwa mwanamke kutosilikizwa na kuteswa na mwanamume ni umapokeo. Hili ni suala linalohusu falsafa ambao ni mhimili wa umuundoleo. Utetezi wa haki za wanawake ulitokana na kuzinduka kwao katika enzi ya usasaleo.

***Utamaduni***

Utamaduni unapingwa na usasaleo kama unadumiza mambo ya kurudisha nyuma jamii. Katika jamii ya mama Hawa mke anateswa na kudhulumiwa bila kusaidiwa na yeyote.Mke alifanya kila njia kumfurahisha mumewe hata anapoteswa.Jamii haionekani kuingilia matatizo katika ndoa hata familia inaposambaratika.Mume anamwacha mkewe na kuoa mwingine anapotaka.Hakuna anayejali hata mtoto.Mtoto anapelekwa kwa ndugu (khalati) bila kutakiwa kutoa maoni yake hata anapokuwa mtu wa miaka kumi na saba alivyokuwa Hawa.

Mtoto kikojozi anabezwa na kuimbiwa wimbo wa dharau kabla ya kuchunguzwa kujulikana usuli wa tabia hii.Watoto wanachapwa hata kama ni wakubwa kama watakosea.Khalati anampiga Hawa makofi mawili ili azungumze. Usasaleo haupingi utamanduni kuendelezwa lakini huhimiza utamaduni usiorudisha nyuma maendeleo ya jamii Farhat (2003). Utamaduni huu ni wa kimapokeo kwa sababu hausaidii kukomboa aila ya Hawa kuteseka. Haya yanapingana na falsafa katika umuundoleo.

**"Mayai Waziri wa Maradhi"**

Hadithi hii iliyoandikwa na Kezilahabi katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* ina maudhui za kiusasaleo.

***Uongozi Mbaya na Kutowajibika***

Mayai Waziri wa Maradhi hawajibiki katika utendaji wake ndiposa: Anasifia maradhi yanayowaangamiza watu wengi.Madaktari anaowasifu ni wale wanaofisha watu.Alipokuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

mwalimu hakuleta usitawi wowote.Shule yake ilikumbwa na migomo mingi.Wizara ya elimu na mchakamchaka aliyoiongoza ilikumbwa na migogoro, kwa mfano, walimu wote wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu waligoma. Ni kiongozi asiye na uzalendo.Anasahau na kukwepa sherehe muhimu za kitaifa. Mayai ana marafiki majangili na wahujumu wa taifa.Hatoi mwelekeo kwa wakulima badala yake huwadhihaki na kuharibu rasilimali; kwenye ndoto anakojoa mtoni.Viongozi kwa ujumla hawajibiki kwa sababu maisha ya wakulima hayajabadilika.Balozi wa Nyumba Kumi anakwepa wajibu na kudai yeye anahusika na wanyama wa porini badala ya binadamu.

Wizara ya biashara na milungula haileti ufanisi wowote ila fursa ya viongozi kufanya magendo.Hakuna wizara inayoshughulikia makao bora ya wananchi,jambo hilo limepuuzwa na wizara inayohusika inabezwa kama ya magofu na utani. Maudhui zinazokejeli siasa na sera za kisiasa katika bara la Afrika ni za kiusasaleo (Kimugung, 2015). Umuundoleo hushughulikia mambo ya kifalsafa katika fasihi.

### *Ushirikina katika Jamaii*

Waziri wa maradhi anadhihirisha kuwa ni mshirikina wakati anapotembelewa na mzuka wa mwanawe. Anatilia shaka kuwa huenda Ukombozi hakufa kifo cha kawaida. Anawatilia shaka wazee waliokuja wakati wa matanga!

> *"Alianza kufikiri kama kweli mtoto wake alifariki au alifanyiwa mazingaombwe?" Anafahamu vyema sehemu zenye waganga mashuhuri yaani Tanga na Bagamoyo. Mayai Waziri wa Maradhi alikuwa radhi na tayari kuwatembelea waganga hao hofu yake ni kwamba angevunja radhi* ( 2004, uk. 68).

Baadhi ya viongozi wa kiafrika kama Mayai huwa na imani ya ushirikina: Huenzi ushirikina na kurudisha nyuma maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia na falsafa ya usasaleo.

### *Utabaka na Siasa za Kiafrika.*

Hii ni hali ya kuwa watu wamegawika katika madaraja tofauti kutegemea mapato hadhi zao na elimu katika jamii (Albert, 1996).

> *Katika ndoto ya kwanza aliota yeye na mawaziri wengine pamoja na wabunge kadhaa wakiwa ndani ya baa wakinywa pombe. Chupa zilikuwa zimejaa mezani na kezi nyingine nyingi zilikuwa zimepangwa pembenei zikiwasubiri. Wanakojoa mtoni sehemu ya juu lakini chini bondeni wakulima waliokuwa wameweka majembe yao pembeni mwa mto walikuwa wanakoga na kusugua miili yao kwa mawe.* (2004 , uk.73).

Wakulima walioweka majembe yao kando ya mto unaokojolewa na walevi wa tabaka la juu wakiwemo wabunge na mawaziri. Wakulima wanajisugua kwa mawe kuonyesha ni watenda kazi kwa bidii lakini hawapati matunda.Wanaofaidika ni wale waliowapa madaraka.Watoto tisa wakondefu na mmoja aliye na afya ni dhihirisho la utabaka.Asilimia kubwa ya wananchi wako katika tabaka la chini na wachache ni wa tabaka la juu.Watoto hao tisa wamevaa mararu, wana njaa na ni dhaifu sana: Ni kinyume na Ukombozi.

Hili ni dhihirisho la kuwepo kwa utabaka. Matokeo ya siasa na sera mbaya za utawala barani Afrika ni utabaka. Matajiri huendelea kutajirika na maskini kuendelea kuwa maskini. Hii ni maudhui ya usasaleo.

### **"Zawadi ya Mume Wangu"**

Hadithi hii imeandikwa na Mohammed (2015) kwa kuzingatia maudhui za kiusasaleo.

### *Fantasia*

Fantasia ni maudhui ya usasaleo; huhusu mapenzi yanayopigwa chuku na ambayo huenda hayafanikiwi. Hadithi inashughulikia wakati mapenzi kati ya Kidawa na Bakari yalikuwa matamu. Bakari anatumia maneno ya kumfurahisha Kidawa. Alimuengaenga kwa maneno "sili silali nisipokuona". Alimwita malkia na akawa anamwimbia nyimbo. Baada ya kufunga ndoa Bakari anabadilika.Kidawa anasema chati ya mapenzi ya Bakari kwake iliteremka na hakumpa nyama ya ulimi tena wala kumwimbia nyimbo.

### *Maisha ya Mjini*

Maisha ya mjini ni maudhui ya usasaleo. Maisha haya hubadilisha tabia ya mhusika. Watu wa mjini

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882

hawarudi nyumbani . Aghalabu hurudi wakiwa na shida: Ni uhakikisho wa ng'ombe anapovunjikia mguu malishoni na kujikokota zizini kusaidiwa. Bakari anapotaka kuhamia mjini Kidawa anakataa na hata kulia. Hawara aliyeonekana kuwa mpenzi wa Bakari wa mjini anapomkabili nyumbani Kidawa anamuwia mkali na kumuuliza uhusiano wake na Bakari.Maneno yake yanamchora mtetezi wa haki za wanawake. Hii ni dhamira moja ya usasaleo.

Mojawapo kati ya magonjwa yanayotokana na maisha ya mjini ni ugonjwa wa ukimwi.Ugonjwa huu huletwa mashambani na watu kutoka mijini. Umuundoleo hutaka mtu achunguze kila jambo. Hupinga kukamilika kwa jambo.

**"Njaa"**

Hadithi hii ina Maudhui za kiusasaleo.

***Imani na Falsafa***

Shule ya Gayaza ilikuwa na madarasa yaliyojaa michoro vichwa vyeusi vya duara. Patti alisema kuwa nyakati nyingine ilikuwa vigumu sana kumwamini Mungu,hasa alipofikiria mambo anayompitisha.Alijiuliza kama kweli Mungu anampenda alipoomba sukari kutoka kwa Linette akanywa chai tamu na yenye uvuguvugu. Alijiuliza vipi Mungu alikuwa na upendeleo kwa baadhi ya watu. Umaskini na uhitaji uanamfanya Patti kushuku Mungu kama asiyejibu maombi yake. Alishuku hata imani yake kwa jumla.

Tapo la usasaleo huhimiza utathmini wa kila jambo ili kugundua kunachokwamiza maendeleo. Huunga mkono mapinduzi. Patti ni mkristo anayetoa ushuhuda lakini ana maswali mengi kuhusu Mungu anayemwabudu. Linette anapomnyima sukari na kumpatia Maria anaonelea kuwa Mungu ana mapendeleo. Mamake anapokosa kumtembelea anasema kuwa wakati mwingine ni vigumu kwake kumwamini Mungu hasa akifikiria mambo aliyompitishia .Anasema kuwa Mungu alikuwa na upendeleo.

***Kutetea Wanyonge***

> *"Ah Mungu! Vipi wewe una mapendeleo. Unawezaje kumpa mwovu vyakula vyote na vitu alivyo na navyo? Mbona nilijitesa kwa kurudi bwenini kunywa chai?"* (2015, uk. 146).

**HITIMISHO**

Makala hii imezingatia mabadiliko ya hadithi fupi za Kiswahili mkabala wa usasaleo. Diwani tatu za hadithi fupi zimetumika ili kubainisha vile hadithi hizi zilivyobadilika mkabala wa usasaleo. Diwani hizi ni *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine na Homa ya Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Mabadiliko ya kimuundo, kimtindo na kimaudhui yalizingatiwa.

Kimuundo; Muundo wa kimapokeo umebainika katika Siku ya Mganga. Huu ni muundo wa kutanguliza mgogoro, maelezo ya mgogoro katikati na mwisho kupatikana kwa suluhu ya mgogoro. Hadithi za 'Jua Litawaka' na 'Njaa' zina muundo wa vipandevipande vya matini ambao ni wa kiusasaleo. Mtindo wa kimapokeo umedhihirika katika hadithi ya 'Kachukua Hatua Nyingine'. Hadithi hii imebainisha usimulizi wa nafsi ya tatu, Istiara ya kawaida na Wahusika wa kawaida. Hadithi za 'Mizungu ya Manabii', 'Mayai Waziri wa Maradhi' na 'Zawadi ya Mume Wangu' zimedhihirisha mbinu za kimtindo za usasaleo. Hizi ni: Istiara iliyotiwa chumvi, uvijimbe, mdondosho mtiririko wa fikra tambuzi, utata na kurudiarudia . Maudhui za kimapokeo zimeshughulikiwa katika hadithi ya 'Kikojozi'. Hizi ni: Kutotetea jinsia ya kike na kutukuza utamaduni. Hadithi za kiusasaleo 'Mayai Waziri wa Maradhi', 'Zawadi ya Mume Wangu' na 'Njaa' zimedhihirisha maudhui za usasaleo. Hizi ni siasa za kiafrika kutetea jinsia ya kike, maisha ya mijini, kutetea wanaokandamizwa falsafa , metafizikia na mapinduzi . Uchunguzi huu utachangia wasomi na wahakiki wa fasihi kuweza kutilia maanani mada ya majaribio , mabadiliko na upya wa kiusasaleo unaojitokeza katika hadithi fupi za Kiswahili za kisasa.

**MAREJEREO**

Arege na wenzake (2012). Mwongozo wa Damu nyeusi na hadithi nyingine. Target Publications.

Amata K. (2005) . Mwongozo wa kipekee na Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine. African DF Network.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.882


Ariel S. (1997). Ecofeminism as politics nature, Marx and the postmodernism. Zed Books.

Babu, O. (2015). Kwambizana kweli katika K. Walibora & S.A. Mohamed, (Wah. ), Homa ya nyumbani na hadithi nyingine (uk. 54 - 62). Phoenix.

Baingana, D. (2015). Njaa. ` Katika K. Walibora & S.A. Mohamed, Homa ya nyumbani na hadithi nyingine ( uk. 141- 152). Phoenix.

Douglas, T. (1993). Nineteenth century American short story. Routledge

Farhat, I. & Wenzake (2003). Postmodern approaches to the Short Story. Greenwood Publishing Group.

Giddens ,E. & Antony, K.(1990). The consequencies of modernity. Standford University.

Habwe J. (2010). Mizungu ya manabii na hadithi nyingine. Phoenix.

Iribemwangi (2011). Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine . EAEP.

Kwambai, M. (2015). Maudhui ya kihalisia katika riwaya dhahania za Katama Mkangi. Tasnifu ya uzamili.(Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Leger, L. (1990). Creating unforgettable characters. Doubley and Company Inc.

Maitaria, J. (2012). Mwongozo wa Damu nyeusi na hadithi nyingine. Longhorn.

March, P.P. ( 2009). The short story an introduction. Edinburgh University Press.

May,C. (1994). The new short story theories . Ohio University Press.

Mbogo, E. (2010). Mizungu ya manabii. Katika J. Habwe (mh.), Mizungu ya manabii na hadithi nyingine ( uk. 32 - 60). Phoenix.

Mohamed , S.A. (2015). Zawadi ya mume wangu. Katika K.Walibora & S.A. Mohamed ( Wah.) . Homa ya nyumbani na hadithi nyingine ( uk. 10-21). Phoenix.

Myszor, F. (2001). The modern short story. Cambridge Universty Press.

Walibora , K. (2007). Atanasi na kismati. Katika K. Walibora & S.A. Mohamed , Kiti cha moyoni na hadithi nyingine (uk. 8-17). Oxford.

Nandwa, R. (2010). Jua litawaka. Katika J. Habwe (mh.), Mizungu ya manabii na hadithi nyingine ( Uk. 190 - 203). Focus Publishers.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa fasihi: nadharia na mbinu. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. & Wafula, R. (2007). Nadharia za uhakiki wa fasihi. Jomo Kenyatta Foundation.

Sacido, J. ( 2012). Modernism and postmodernism and the short story. Longman Green.

Timammy, R. (2010). Kikojozi. Katika J. Habwe (mh.), Mizungu ya Manabii na hadithi nyingine ( uk. 180 - 188). Phoenix.

Timammy, R. (2004). Uteuzi wa moyoni. Katika Wamitila, K.W. (mh.), Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine ( uk. 7-19). Focus Publishers.

Wamitila, K. (2003). Kamusi ya fasihi ; istilahi na nadharia. Focus Publications.

Wamitila, K.W. (2004). Kachukua Hatua Nyignine . Katika K.W. Wamitila Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine ( uk. 38 - 49). Focus Publishers.

Williams, R. (1995). The postmodern novel in Latin America. Politics, culture and crisis of truth. St. Martin’s .


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.